28 Oktoba 2015

TOLEO LA 18 LA SEKTA YA ARDHI

MAREKEBISHO YA ARDHI NCHINI: SHERIA MPYA ZA ARDHI MWAKA 2015

I. Hali ilivyo

Bunge hivi maajuzi iliongeza kwa mwaka mmoja muda unaohitaji ili kuweza kupitisha sheria makhsusi chini ya ratiba ya tano ya katiba ya Kenya ya mwaka 2010. Miongoni mwa sheria hizi ni zile zinazohusiana na maswala ya ardhi ambazo ni: Sheria ya ardhi mwaka 2012, sheria ya usajili wa ardhi mwaka 2012, na sheria ya tume ya kitaifa ya ardhi mwaka 2012.

Kulingana na ratiba ya tano inayotoa mwelekeo wa sheria zitakazopitishwa na bunge baada ya kupitishwa kwa katiba mnamo mwaka wa 2010, sheria zihusianazo na ardhi ya kijamii, (Kifungu cha 63 cha katiba 2010) na matumizi ya ardhi sawa na mali (kifungu cha 66 cha katiba 2010) zilipewa kipindi cha miaka mitano kupitishwa. Baada ya kupitishwa kwa sheria kadhaa mnamo mwezi Aprili mwaka wa 2012, taifa hili lilikuwa na kipindi cha miaka mitatu kupitisha sheria hizo zihusianazo na ardhi ya kijamii sawia na matumizi ya ardhi na mali. Hata hivyo haya hayakushuhudiwa kwani mnano Agosti 2015, baada ya kumalizika kwa muda uliotolewa na katiba, sheria hizi ziliorodheshwa miongoni mwa zile zilizochelewa kupitishwa. Kufuatia hali hii sheria hizi zinastahili kupitishwa katika kipindi cha mwaka mmoja ujao baada ya bunge la kitaifa kuongeza muda huo.

Ni vyema kutambua na kushukuru bunge kwa kujizatiti kupata maoni ya wadau kuhusiana na sheria ya ardhi ya kijamii ya mwaka 2015 (kifungu cha 63) sheria ya mipango ya maeneo ya mwaka wa 2015 (kifungu cha 66) na sheria ya marekebisho ya sheria za ardhi ya mwaka wa 2015. Hivi karibuni bunge linatarajiwa kuendeleza mijadala kuhusiana na mapendekezo haya ya sheria hizi muhimu. Hatua hii itasaidia kuepuka uwezekano wa kuwasilisha sheria hizi mwaka ujao. Hasa ikizingatiwa kuwa siasa za humu nchini tayari zitakuwa zikichochea uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2017 na hivyo basi huenda sheria hizi zikachukua mwelekeo wa kisiasa.

II. Chapishi/Nakala tofauti za sheria ya ardhi ya kijamii

Japo taasisi hii inafahamu fika kuwa tayari sheria ya ardhi ya kijamii ya mwaka 2015 (bunge la kitaifa No 45) inasubiri mjadala katika bunge la kitaifa, chapishi/nakala tofauti ya sheria hii ya ardhi ya kijamii, (Bunge la senet, No 38 ya mwaka 2014) pia inasuburi kujadiliwa katika bunge la senet. Taasisi hii hivyo basi inatoa wito kwa bunge kutatua sintofahamu hii inayohusiana na sheria hii muhimu na kuhakikisha kunao upatanisho utakaosaidia wadau na wabunge kwa jumla kujadili sheria hii ya ardhi ya kijamii.

Aidha ni tumaini ya taasisi hii kuwa bunge litaendeleza kasi iliyoshuhudiwa ili kuwezesha sheria hizi za ardhi kupitishwa haraka iwezekanavyo kwa minajili ya kuanza kutumiwa na wakenya. Hata hivyo bunge linastahili kuchunguza kwa kina sheria hizi kabla ya kuzipitisha ili kuona kwamba zinaambatana, na katu hazihitilafiani kisheria. Haya yatasaidia kuepuka migogoro miaongoni mwa taasisi husika kama ilivyoshuhudiwa siku zilizopita.

III. Yaliojitokeza na Mapendekezo muhimu

Baada ya mwito kutolewa na kamati ya ardhi katika bunge la kitaifa, taasisi hii ilichangia pakubwa katika kila moja ya sheria hizi za ardhi mapema mwezi Septemba mwaka wa 2015. Tumaini lililopo ni kuwa michango hii pamoja na ile iliyotolewa na wadau wengine itazingatiwa ili kuboresha sheria hizi. Kwa jumla taasisi hii ingependa kusema hivi.

1. ***Ni vyema kupunguza vikamilifu sheria na taasisi za ardhi**:* Wakati wa kupitisha sheria za ardhi, bunge linastahili kuongozwa na nguzo ya kupunguza kikamilifu sheria hizi za ardhi. Ni vyema pia kwa bunge kuwa makini na kuzuia ustawishaji wa taasisi nyingi za ardhi kwani kando na kuongeza gharama ya kuziendesha, wateja ambao ni wakenya mara kwa mara wanahisi kuchoshwa na uwepo wa taasisi nyingi zihusianazo na maswala ya ardhi. Mara nyingi wateja hawa hushindwa kutambua ni taasisi ipi inajihusisha na huduma zipi.
2. ***Mjadala wa umma unakaribishwa**:* Mjadala wa kina kuhusiana na sheria za ardhi ni jambo muhimu kwani unasaidia pakubwa kutoa hamasisho kwa umma na ni msingi bora hata kwa utekelezaji wa sheria hizi.
3. ***Jumulisha taratibu za bunge la kitaifa na la senet katika sheria ya ardhi ya kijamii**:* Ili kuwezesha mijadala na michango bora katika sheria ya ardhi ya kijamii ni vyema taratibu za bunge la kitaifa na zile za bunge la senet kujumulishwa.
4. ***Michango ya wadau**:* Wadau wanastahili kunyakuwa fursa iliyopo ili kuchangia sheria husika ikizingatiwa tarjiba kuu walionayo katika Nyanja mbali mbali za usimamizi wa ardhi nchini. Kamati ya ardhi bungeni inapaswa kuzingatia kwa makini mawasilisho ya

kila moja ya sheria hizi, kwani ni kwa misngi ya utofauti huu ndipo sheria bora zitabuniwa.

5. ***Sheria ya ardhi ya kijamii****:* Zaidi ya asilimia 60 ya mtaji wa ardhi nchini ni ardhi ya kijamii ambayo bado haijasajiliwa. Hivyo basi ni bora kwa haraka kuwa na sheria itakayo saidia kutambua, kusajili, kusimamia, na kutekeleza yote yahusianayo na ardhi ya aina hii yakiwemo mikakati ya uwekezaji. Huku kukiwepo na haja kubwa ya uwekezaji katika ardhi ya kijamii, kwa minajili ya uchimbaji mafuta na madini , ustawishaji wa miundo mbinu, na ikizingatiwa kuwa katiba katika Kifungu cha 63 (d)(4) inasema kuwa ardhi ya kujamii haiwezo twaliwa ila kwa misngi ya kisheria inayoratibisha kiwango na haki za wenyeji wa jamii hiyo husika kwa umoja au kwa ujumla, ni sharti tuharakishe uetekelezaji kwa sheria hii ya kimsingi.
6. ***Sheria ya mipango ya maeneo/asili****:* Sheria hii itasaidia kuimarisha mipango, matumizi, usimamisi wa kisheria na ustawishajiwa ardhi nchini, na hivyo basi ni muhimu kwa kutoa mwelekeo wa ustawishaji wa kasi wa maeneo yetu ya mijini sawa na yale ya mshambani.
7. ***Sheria ya marekesbisho ya sheria za ardhi****:* Sheria hii inasaidia kusuluhisha migogoro ya mara kwa mara kati ya wizara ya ardhi, nyumba na mipango na tume ya kitaifa ya ardhi. Aidha inajumuisha miongozo ya kupokea, kuchunguza na kupendekeza suluhu za unyanyasahi wa kihistoria, kusimamia ufurushwaji katika kila kitengo cha ardhi na kumudu viwango vya umiliki wa ardhi. Uchunguzi wa taasisi hii uliofanywa mnamo mwezi Mei mwaka wa 2014 kuhusiana na vipengee vinavyohitilafiana kwenye katiba ya mwaka 2010, na sheria za ardhi, usajili wa ardhi na tume ya kitaifa ya ardhi, na ambavyo vimepelekea kuwepo kwa migogoro, migogoro ambayo sheri hii ya marekebisho inalenga kutatua, miongoni mwa maswala mengine unapatikana katika tuvuti hii. www.ldgi.org/ www.ldgi.co.ke.
8. ***Kuputishwa kwa sheria za ziada****:* Punde tuu bunge litakapopitisha sheria za ardhi zilizosalia, ni vyema izidishe kasi ya kupitisha sheria za ziada zitakazosaidia utekelezaji wa sheri za ardhi za mwaka 2012 na 2015.

Imetolewa na Taasisi ya Ustawishaji na Usimamizi wa Ardhi tarehe 26 Oktoba 2015